**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

## KISWAHILI SEHEMU A

Gredi ya 8

NAKALA YA MWANAFUNZI

**SEPTEMBA 2024**

© KNEC 2024

**GEUZA UKURASA**

Mtu anapougua hutafuta matibabu kutoka kwa dakatari. Kwa kawaida, daktari humwandikia mgonjwa huyo dawa zifaazo baada ya kumfanyia uchunguzi. Inatarajiwa kwamba mgonjwa akishaandikiwa dawa atazitumiwa kulingana na maagizo. Asipofanya hivyo huenda dawa hizo zikakosa kufanya kazi iliyokusudiwa au hata kumdhuru.

Zipo dawa za aina mbalimbali. Kuna zile ambazo humezwa, za kutiwa kwenye sehemu zenye maumivu, za kupakwa na hata za kudungwa kwa kutumia sindano.

Ili kuhakikisha matumizi yaafayo ya dawa, jamii inashauriwa kuzingatia maagizo ya daktari. Kwa mfano, kutumia dawa kwa viwango vilivyopendekezwa, kuzitumia kwa wakati ulioagizwa na kutogawa dawa kwa wagonjwa wengine. Isitoshe, tunafaa kuongeza kiasi cha maji kinachofaa kulingana na maelekezo. Tufahamu kuwa si vyema kununua dawa bila ushauri wa daktari.

Aidha, wanajamii wanatahadharishwa dhidi ya kuweka dawa ovyoovyo. Inastahili kuzihifadhi mahali palipo salama na mbali na watoto.